
KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
REVISION MOCK EXAMS 2016
TOP NATIONAL SCHOOLS

MANG'U HIGH SCHOOL
KISWAHILI
KARATASI YA 3

SCHOOLS NET KENYA
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetworkkenya.com

MANG'U HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

102/3

FASIHI

KARATASI YA TATU

SEHEMU A: USHIAIRI

SWALI LA LAZIMA

1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

LONGA

Longa Longea afwaji, watabusarika,
Longa uwape noleji, watanusurika,
Longa nenea mabubu, sema na viduko.

Longa usichachawizwe, tamka maneno,
Longa usitatanizwe, mbwa aso meno,
Longa usidakihizwe, kishindo cha funo.

Longa yote si uasi, si tenge si nomá,
Longa pasi wasiwasi, ongea kalima,
Longa ukuli kwa kasi, likate mtima,
Longa zungumza basi, liume ja uma.

Longa japo ni kombora, kwa waheshimiwa,
Longa liume wakora, kwani wezi miwa,
Longa bangu na papara, hawakuitiwa,
Longa bunge si kiwara, si medani tawa,
Longa ni simbamarara, wanaturaruwa.

Maswali

- (a) Tambua nafsineni katika nudhumu hii. (alama 1)
- (b) Onyesha vile kibali cha utunzi wa mashairi kiliviyotumiwa kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
- (c) Kwa kutoa maelezo mwafaka, tambua bahari **nne** zilizotumiwa na mtunzi kwenye shairi hili. (alama 8)
- (d) Onyesha vile shaha alivyofua dafu kutumia mbinu zifuatazo. (alama 5)
- (i) Anafora
 - (ii) Usambamba wa kiusawe.
- (i) Usambamba wa kifahiwa/dhamira.
- (ii) Tabaini.
- (iii) Jazanda
- (e) Tambua toni ya shairi hili. (alama 1)

- (f) Neno kasi ni adhidadi. (alama 1)
(g) Neno awaji limetumika kumaanisha nini katika shairi hili. (alama 1)

SEHEMU B: MSTAHIKI MEYA

2. "Mimi na Meya ni mfano wa mafuta na maji. Hatuonani uso kwa uso."
(a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
(b) Ni mbinu gani ya lugha iliyotumika katika dondo na inamaanisha nini? (alama 2)
- (c) Kwa kurejelea tamthilia nzima, thibitisha kuwa Meya ni sawa na mafuta na wengine ni maji. (alama 14)

AU

3. Thibitisha ukweli wa msemo kuwa sikio la kufa halisikii dawa kwa mujibu wa Tamthilia ya Mstahiki Meya (alama 20)

SEHEMU C: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

KANDA LA USUFI

4. "Wanafunzi hao wawili waliandamana hadi ilipokuwa kliniki ya shule."
(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
(b) Kwa kurejelea hadithi kanda la usufi thibitisha kuwa sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto myingi. (alama 10)
- (c) Wanafunzi wanaorejelewa walikuwa wamekutana kisadfa. Toa mifano mingine **mitatu** ya sadfa kutoka kwenye hadithi hii. (alama 6)

AU

5. **MIZIZI NA MATAWI**

Thibitisha kuwa majina Sudi na Kudura ni ya kimajazi. (alama 20)

SEHEMU YA D: KIDAGAA KIMEMWOZEA

6. Mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea amenuia kujenga jamii mpya. Tetea kauli hii. (alama 20)
- AU**
7. "Hatimaye Tarishi alikuja na barua moja ya Mtemi na nakala ya siku hiyo ya gazeti la Tomoko Leo: Mtemi Nasaba Bora akapokea barua hiyo na gazeti toka kwa tarishi aliyekuwa kanywea si haba."

- (a) Jadili mambo yaliyomshua Mtemi Nasaba Bora kuhusiana na barua na gazeti alizopokea siku hiyo. (alama 10)
(b) Onyesha jinsi madhubuti alivyoendeleza uasi dhidi ya babake. (alama 10)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Maigizo ni nini? (alama 2)
(b) Fafanua sifa zozote **tano** za maigizo. (alama 10)
(c) Eleza dhima ya michezo ya watoto. (alama 8)